


UNACHOHITAJI KUFANYA NA MATOKEO YA KIPIMO CHAKO CHA COVID-19 CHA NYUMBANI



Matokeo chanya ya kipimo

Kaa nyumbani kwa siku 5
(kwa waliochanjwa na wasiochanjwa)



Kaa nyumbani katika chumba ambapo uko mbali na wengine wanaoishi nawe.



HUNA haja ya kupata kipimo cha ziada cha PCR



Ikiwa huna dalili baada ya **SIKU 5**, unaweza kuondoka kwenye nyumba yako **LAKINI** uvae barakoa kwa siku 5 zaidi.

Ikiwa una homa, endelea kukaa nyumbani hadi homa yako iishe kwa saa 24



Ili kuzuia kuenea kwa COVID, mjulishe mtu yeyote uliyekaribiana naye hivi majuzi na umhimize apimwe, fuatilia kwa ajili ya dalili na upunguze kuwahatarisha watu wengine.

Matokeo hasi ya kipimo

Una Dalili

(kwa waliochanjwa na wasiochanjwa)



- Kikohozi
- Homa/Baridi kali
- Kukosa pumzi
- Maumivu ya misuli au mwili
- Kutapika, kuhara
- Upotezaji mpya wa hisia ya kuonja au kunusa

Ikiwezekana, pata kipimo cha PCR AU Urudie kipimo cha nyumbani baada ya siku 1-2



Kaa nyumbani hadi ujue matokeo ya kipimo chako.

Ukipatikana kuambukizwa, fuata miongozo ya matokeo chanya.

Ukiwa matokeo ni hasi tena, hakuna kipimo kingine kinachohitajika wakati huu.

Ikiwa huwezi kupimwa, chukulia kwamba umeambukizwa na ukae nyumbani

Huna Dalili

(inategemea hali ya chanjo; angalia hapa chini)

Hakuna kipimo kingine kinachohitajika kwa wakati huu, isipokuwa:

Ikiwa ulikaribiana na mtu aliyearchukiziwa COVID-19:

Ikiwa umepata dozi zote za chanjo unazostahiki*:

- Vaa barakoa ukiwa karibu na wengine kwa SIKU 10
- Pima katika Siku ya 5 ikiwezekana

Ikiwa hujachanjwa, hujamaliza chanjo au hujapata nyongeza (hujapata dozi zote)

- **Kaa nyumbani kwa SIKU 5**
- Kisha vaa barakoa ukiwa karibu na wengine kwa SIKU 5 ZAIDI
- Pima katika Siku ya 5 ikiwezekana

Ukipata dalili, kaa nyumbani na uende kwenye safu wima ya "NINA DALILI"

Iwapo una maswali yoyote, tafadhali tembelea cv.nmhealth.org/selftest au piga simu kwa Nambari ya Simu ya Dharura ya Virusi vya Korona: 1-855-600-3453

